



Ubora wa chanjo ya malaria ya MSP3 kwa watoto wa Kwashemshi, Korogwe wenye umri wa miezi 12-24



Taasisi zinazohusika

Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu, Kituo cha Tanga, Tanzania (NIMR-Tanga centre)

Taasisi ya Afya na Magonjwa ya Ukanda wa Joto, Uingereza, (LSHTM-UK)

Taasisi ya Mtandao wa Chanjo Afrika, Dar es Salaam, Tanzania (AMANET)

Taasisi ya Pasteur Paris, Ufaransa (Institut Pasteur Paris, France)

Utangulizi

Ugonjwa wa malaria ni tatizo kubwa katika jamii yetu hasa kwa watoto chini ya miaka mitano. Zipo njia mbalimbali za kujikinga na malaria ambazo ni usafi wa mazingira na kuondoa mazingira ya mazalia ya mbu, kujikinga kuumwa na mbu hasa kwa kutumia chandarua chenye viuatilifu au kupuliza dawa za kuuu mbu na kujipaka dawa zinazozuia mbu kukaribia ngozi, kutumia dawa ambazo zinaua vimelea vya malaria kwa pale ambapo mtu anamwa kama vile dawa mseto (ALU). Njia nyingine ya kujikinga na malaria ni kwa kutumia chanjo za malaria.

Chanjo za malaria hivi sasa bado zipo katika ngazi mbalimbali za majaribio. Miongoni mwa chanjo hizo ni MSP3 ambayo ilishafanyiwa majaribio Ulaya, Marekani na Afrika Magharibi (Burkina Faso). Kwa mara ya kwanza majaribio haya yamefanywa hapa kwetu Tanzania katika kijiji cha Kwashemshi, Kata ya Vugiri, Tarafa ya Bungu, Wilaya ya Korogwe, Tanga.

Utaratibu

Utafiti huu wa chajo ya malaria ya MSP3 ulianza mwezi Agosti 2007 ambapo baada ya **makubaliano na wananchi wa Kwashemshi, kupitia viongozi**

wao na wanakijiji wote kwa ujumla, yafuatayo yalifanyika:

Ujenzi wa jengo la kutolea chanjo pamoja na huduma za tiba.

Tathmini ya afya ya watoto wapatao 56 ambapo waliohitajika ni 45.

Utoaji wa vipimo vya damu ili kutathmini hali za afya za watoto hao.

Utoaji wa chanjo tatu kwa kila mtoto (ambapo wote 45 walishiriki na kupata chanjo zote tatu).

Ufuatiliaji wa watoto baada ya chanjo na siku sita baada ya chanjo.

Uwepo wa matabibu hapa kijijini ambao walitoa huduma wakati wowote walipohitajika.

Uwepo wa huduma za usafiri na endapo yeyote aliumwa na tiba haikupatikana kijijini alipelekwa katika Hospitali ya Wilaya ya Korogwe (maarufu kama Magunga).

Hatimaye, utafiti huu ulifikia kikomo mwezi Novemba 2008.

Matokeo

Ushiriki ulikuwa wa kuridhisha na wa hiari.

Hakuna madhara yaliyojitokeza kutokana na chanjo hii.

Ubora wa chanjo hii ni sawa na chanjo zinazotolewa ili kuzuia magonjwa mengine kama vile homa ya ini.

Hivyo basi matokeo haya tumeyatoa kwenye mkutano wa kisayansi kule Marekani na tutachapisha kwenye majarida ya kisayansi.

Wadau wengine miongoni mwao wakiwa ni Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na AMANET (African malaria Network Trust) wameshapewa matokeo ya utafiti huu

Hitimisho

Chanjo hii ya MSP3 ni bora na salama (safe) na pia inachochea mwili kutengeneza kinga dhidi ya vimelea vya malaria (immunogenic). Tunatarajia kuwa, wafadhili wetu (AMANET) watatuwezesha kufanya mradi mwingine wa awamu ya kwanza au ya pili wa chanjo ya MSP3 (MSP3 phase 1b/2b) hapo baada.

Shukurani

Mradi huu unapenda kutoa shukurani za dhati kwa washiriki (watoto) kupitia kwa wazazi/walezi wao kwa kuridhia kushiriki katika utafiti huu. Tunatoa shukurani kwa wanajamii na viongozi wa kijiji cha Kwashemshi kwa ushirikiano wao mkubwa. Vilevile tunatoa shukurani kwa Taasisi ya AMANET kwa kufadhili mradi huu. Tunapenda kutoa shukurani zetu za dhati kwa Profesa Pierre Druilhe wa Paris, Ufaransa kwa ugunduzi wa chanjo na utengenezaji wa chanjo hii ya MSP3 na kutupatia kuifanyia majaribio ya utafiti. Tunaishukuru Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii pamoja na Taasisi ya Taifa ya Utafiti wa Magonjwa ya Binadamu pamoja na uongozi wa wilaya ya Korogwe kwa kuturuhusu kufanya utafiti huu.